BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,
Buyu,
70490 Mjini Magharibi,
S.L.P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 2242000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAJUMUISHO YA MIJADALA YA BAJETI ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua fursa hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa kuanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na uzima pamoja na Wajumbe wenzangu wote ambao tumekutana leo kuendelea kutekeleza majukumu yetu katika hali ya amani na utulivu. Aidha, napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika pamoja na wasaidizi wako wote kwa namna mnavyoliongoza vyema Baraza hili na tukaweza kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima naomba kumpongeza Mheshimiwa Dkt Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kutuongoza kwa umahiri mkubwa na kuiletea maendeleo nchi yetu. Mafanikio ambayo tunaendelea kuyapata ni kutokana na mashirikiano mazuri ambayo Mheshimiwa Rais amekuwa akiyapata kutoka kwa wasaidizi wake wote wakiwemo wasaidizi wa karibu Makamo wa Kwanza wa Rais, Mhe. Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Hemed Suleiman Abdulla. Kwa pamoja tunawapongeza sana kwa utendaji wao.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa busara na hekima zao wanazozitumia katika kutekeleza shughuli za Kamati hasa kwa kunishauri vyema kuiongoza Kamati hii pamoja na kuishauri Serikali. Naomba kuwatambua Wajumbe hao na makatibu kwa kuwataja kama ifuatavyo:

1. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma — Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Soud Nahoda Hassan — M/Mwenyekiti

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Mhe. Rukia Omar Ramadhan | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Asha Abdulla Mussa | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mohamed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Suleiman Masoud Makame | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Yussuf Hassan Idd | Mjumbe |
| 9. | Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 10. | Ndg. Abass Vuai Moh'd | Katibu |
| 11. | Ndg. Husna Rajab Othman | Katibu, na |
| 12. | Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa Hotuba hii ya Majumuisho ya MIjadala Ya Bajeti za Wizara ni matakwa ya Kanuni ya 101(2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020) ambayo inaielekeza Kamati ya Bajeti kwa kushauriana na Serikali kufanya majumuisho ya hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili Bajeti za Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kukujuulisha kwamba, katika Mkutano huu wa Kumi na Tano wa Baraza la Wawakilishi ambao ajenda yake kuu ni upitishaji wa Bajeti za Wizara na Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025, hoja zote za kibajeti zilizoibuka zilipatiwa ufafanuzi wa kutosha Barazani na hivyo hakukuwa na hoja za kibajeti zilizoletwa katika Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa mijadala ya Bajeti za Wizara, baadhi ya maeneo yalichangiwa na Wajumbe wengi zaidi na baadhi ya maeneo hayo yalichangiwa kwa hisia na msisitizo mkubwa. Kwa lengo la kuikumbusha Serikali ili kuichukulia michango hii kwa uzito maalum na kwa kuwa hii ni hotuba ya majumuisho ya mijadala ya bajeti, Kamati yangu imeona ni vyema kuchukua fursa hii kuyapa uzito maeneo hayo kwa kuyakumbushia Pamoja na kutoa ushauri kwa Serikali ili iweze kuyafanyia kazi kwa weledi na kwa haraka na hatimae kufikia malengo ya kupata ufanisi katika utekelezaji wa bajeti zetu sambamba na kutoa huduma bora kwa wananchi. Maeneo hayo ni kama yafuatayo:

## Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais

**Mheshimiwa Spika,** Mfumko wa bei ni eneo ambalo lilichangiwa na Wajumbe wengi ambapo walieleza kwamba mfumko huo wa bei unaathiri zaidi bidhaa za chakula ambazo matumizi yake ni ya msingi na wananchi hulazimika kuzitumia kila siku.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kutatua changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kusimamia suala la mfumko wa bei na kuhakikisha inaweka mikakati thabiti ili kuudhibiti ikiwemo kufanya mabadiliko katika sekta ya kilimo na kuelekea katika kilimo cha kisasa kitakacholeta tija zaidi kwa kuongeza uzalishaji wa chakula nchini ili kupunguza kutegemea kuagiza chakula.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa suala hili la mfumko wa bei hasa katika bidhaa za chakula limekuwa linazungumzwa mara nyingi na kiukweli linawaathiri wananchi hasa wa kipato cha chini, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kuzisimamia Sheria zetu za Uwekezaji na kuzifanya rafiki ili ziweze kushawishi uwekezaji wa viwanda utakaopelekea nchi kuweza kuzalisha zaidi pamoja na kuweza kuuza nje na kupata fedha za kigeni. Aidha, suala la kuongezwa thamani kwa mazao yanayozalishwa nchini nayo litatoa fursa za ajira kwa vijana katika maeneo yatakayofunguliwa viwanda kwa ajili ya kuongeza thamani katika bidhaa za kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine ambalo lilichangiwa na Wajumbe wengi ni eneo linalohusiana na maafa ambapo wajumbe waliitaka Kamisheni ya Maafa kuisaidia jamii wakati maafa yanapojitokeza. Licha ya uhaba wa fedha katika Kamisheni hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha kukabiliana na maafa pamoja na kuendelea na taratibu za kuandaliwa kwa kanuni itakayopelekea Kamisheni kuwa na uwezo wa kuanziasha Mfuko wa Maafa utakaochangiwa na Serikali, wafanyabiashara, wahisani mbali mbali na mashirika ya Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine Kamati inawanasihi wananchi kufuata taratibu zote zinazoelekeza maeneo sahihi ya makazi pamoja na kujiepusha na tabia ya uvamizi wa maeneo ambayo si rasmi kwa ajili ya makaazi ambayo kwa kiasi kikubwa ndio yanakumbwa na maafa.

## Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa Mjadala wa Bajeti ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Wajumbe wengi walichangia suala la changamoto kuwepo ya uharibifu wa mazingira unaochangiwa na shughuli za kiuchumi ikiwemo uchimbaji mchanga na mawe. Wananchi hujishughulisha na kazi hizo ni kwa ajili ya kujipatia kipato ili kukidhi mahitaji yao mbali mbali.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kukabiliana na hali hii, Kamati inaishauri Serikali kuendelea na usimamizi wa maeneo yanayostahiki kufanywa uchimbaji wa mawe na mchanga pamoja na kuendelea kuwapa elimu wananchi kuhusu namna bora ya utunzaji wa mazingira kwani ni suala muhimu kwa maisha yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Suala jengine lililochangiwa na Wajumbe wengi ni kuhusiana na utaratibu wa kuwapatia mikopo watu wenye ulemavu. Kwa kuwa utaratibu uliopo sasa unahitaji watu wenye ulemavu wajiunge katika vikundi vya watu watano ili waweze kupatiwa mikopo hiyo. Kutokana na sharti hili imekuwa ni vigumu sana kupatikana kwa vikundi hivyo hasa ukizingatia kuwa ulemavu upo wa aina tofauti na sio rahisi kuweza kupata kikundi cha watu hao wenye mawazo yanayofanana katika kuendeleza fedha za mikopo hiyo katika shughuli za kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri watu wenye ulemavu wapatiwe mikopo baada ya kukidhi masharti mengine ya msingi na sio lazima kufanya vikundi kwani kufanya hivyo kutapelekea kuendeleza shughuli zao za kiuchumi, kuongeza kipato na kupunguza utegemezi katika mahitaji yao mbali mbali.

## Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

**Mheshimiwa Spika,** Suala la kuharakisha ujenzi wa ofisi za masheha lilichangiwa na Wajumbe wengi na kwa kweli jambo hili ni la msingi sana kwani kwa kipindi kirefu masheha wamekuwa wakifanya kazi katika nyumba zao. Kamati inaunga mkono jambo hili na kuitaka Serikali kusimamia ujenzi wa ofisi hizo ambazo zitatoa fursa kwa masheha wetu kuweza kutekeleza majukumu yao katika mazingira mazuri na kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wengi waliipongeza Serikali kwa kutekeleza Miradi ya Ujenzi wa Masoko ambayo yataweza kutoa fursa kwa wananchi katika kutekeleza shughuli zao za kiuchumi pamoja na kupata huduma wanazozihitaji katika masoko hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Masoko ya Jumbi, Chuini na Mwanakwerekwe, Wajumbe walisisitiza sana juu ya umuhimu wa Serikali kufanya ufunguzi wa masoko hayo kwa haraka pamoja na kuzingatia uendeshaji wake, utaratibu wa kuyafanyia ukarabati kwa muda utakaohitajika pamoja na kuangaliwa utaratibu ulio wazi katika ugawaji wa sehemu za kufanya biashara kwa wananchi wanaohitaji.

## Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi

**Mheshimiwa Spika,** Katika mjadala wa bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Wajumbe wengi walichangia kwa msisitizo suala la maendeleo ya Miradi ya Ujenzi wa Barabara, na msisitizo zaidi ulielekezwa katika Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Chake – Wete kutokana na Wajumbe wengi kuonesha kutoridhishwa na utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuingia mikataba mizuri baina yake na Wakandarasi pamoja na Washauri Elekezi, mikataba ambayo italinda maslahi ya nchi pale ambapo itatokea changamoto ya kutokutekelezwa kazi za ujenzi kwa ufanisi kwani mikataba huelezea misingi ya utekelezaji wa miradi na kifanyike kitu gani iwapo kutatokea changamoto yoyote. Aidha, Serikali ihakikishe inatoa zabuni kwa wakandarasi makini wenye sifa na uwezo wa kutekeleza miradi kwa ufanisi na kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine ambalo limesisitizwa ni kuwepo kwa ajali nyingi zinazosababishwa na usafiri wa bodaboda. Kamati inaishauri Serikali kusimamia sheria za usalama wa barabarani kwa ufanisi, bila ya kuwa na muhali. Aidha, tunawanasihi wazazi kutozifanya bodaboda kuwa mabasi ya kupakia wanafunzi (school buses) na inapobidi idadi na tahadhari ichukuliwe kwa mujibu wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine ambalo Wajumbe walichangia kwa msisitizo ni kuchelewa kuanza utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Mangapwani, Wete na Shumba. Kamati imeridhika na majibu ya Serikali kwamba inaendelea na taratibu za kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji katika miradi hiyo. Sambamba na

hilo, Kamati inaisisitiza Serikali kuongeza kasi ya utafutaji fedha hizo ili miradi hiyo ianze kutekelezwa kwa haraka.

### Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

**Mheshimiwa Spika**, Katika Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Wajumbe wengi walichangia suala la kukuza lugha ya Kiswahili. Kamati inashauri kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ili wafahamu kwamba lugha ya Kiswahili ni muhimu kwa utambulisho wa Taifa na urithi wa utamaduni wa Zanzibar. Vile vile Serikali itoe motisha kwa waandishi wa vitabu na wanahabari kuandika kazi zao kwa Kiswahili, na kuendeleza programu za kutafsiri kazi muhimu za kitaaluma na kisayansi kwa Kiswahili.

**Mheshimiwa Spika**, Sambamba na hilo, Serikali isaidie katika ufadhili wa tafiti kuhusu Kiswahili na matumizi yake katika teknolojia mpya ili lugha hii iweze kufuatilia mabadiliko ya ulimwengu wa kisasa. Aidha, kutafuta fursa za kusomesha lugha ya Kiswahili nje ya nchi kutasaidia kukuza lugha hii na kueneza utamaduni wa Kiswahili duniani.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imekuwa ikishauri mara nyingi kuhusiana na suala hili la kutafuta fursa ya kusomesha Kiswahili nje nchi, na inaendelea kuishauri Serikali kuwapa mafunzo ya namna ya kusomesha lugha za kigeni kwa vijana wenye ujuzi wa lugha ya Kiswahili na baadae kuwaunganisha na vyuo nje au nchi ambazo zinahitaji walimu wa Kiswahili. Hatua hii itasaidia pia kukuza uchumi wetu kwa kutoa ajira kwa vijana wengi hususan waliyomaliza vyuo vikuu.

**Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Vijana kutopata fedha za maendeleo inapelekea miradi ya vijana kushindwa kutekelezwa na hivyo kuwanyima vijana fursa muhimu za kujikwamua kiuchumi na kijamii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali, katika utekelezaji wa Programu za Maendeleo ya Vijana, ihusishe Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA) na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ili ziende sambamba na uwezeshaji wa vijana kwa kutoa mikopo, mafunzo ya amali pamoja na kuanzisha vikundi vya ubunifu hususan katika TEHAMA kwa vijana waliomaliza vyuo vikuu. Programu hii ikitekelezwa kwa ufanisi na kimkakati itasaidia kuwawezesha vijana kupata fursa za kiuchumi, kukuza ujuzi wao na kuchangia maendeleo ya jamii kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine lililochangiwa na Wajumbe wengi katika Wizara hii ni kuhusu kulinda utamaduni na kuzingatia maadili ya Mzanzibari kutokuathiriwa na wageni wanaokuja Zanzibar. Kamati inaishauri Serikali, kuchukua hatua zifuatazo: **Kwanza,** Kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kulinda utamaduni na maadili kupitia vyombo vya Habari katika skuli na katika mikutano ya kijamii. **Pili,** Kutengeneza na kutekeleza Sheria na Kanuni zinazolinda utamaduni wa Mzanzibar. **Tatu,** Kutoa mafunzo kwa wananchi hususan vijana, kuhusu njia bora za kuamiliana na wageni bila kupoteza utamaduni wetu. **Nne,** Serikali iwashirikishe Viongozi wa kidini kikamilifu katika kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kulinda maadili na utamaduni na **Tano** Kuendeleza utalii unaoheshimu na kuzingatia utamaduni wa Zanzibar kwa kuwahimiza watalii kufuata maadili na tamaduni za Zanzibar.

## Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale

**Mheshimiwa Spika,** Zanzibar ni maarufu kwa vivutio vyake vya utalii kama vile fukwe nzuri, historia tajiri na utamaduni wa kipekee. Suala la kuimarisha na kuvitangaza vivutio vya utalii ili kuongeza idadi ya wageni wanaotembelea Zanzibar limesisitizwa sana na Wajumbe walipokuwa wakichangia Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale. Ili kuimarisha utalii Zanzibar, Serikali inapaswa kuendelea kuimarisha miundombinu ya barabara, usafiri, na huduma za afya, kuanzisha kampeni za matangazo kimataifa kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii na kutoa mafunzo kwa watoa huduma za utalii ili kuimarisha ubora wa huduma.

**Mheshimiwa Spika,** Pia, ni muhimu kuhifadhi na kuendeleza maeneo ya kihistoria na asili, kushirikiana na sekta binafsi, kutambua masoko mapya, na kufanya utafiti wa mara kwa mara ili kuelewa mahitaji ya watalii. Kwa kuchukua hatua hizi, Zanzibar itaweza kuongeza idadi ya watalii na kuimarisha uchumi wake kupitia sekta ya utalii.

**Mheshimiwa Spika,** Suala la kuimarisha huduma za kijamii hususan maji na nishati katika maeneo ya vivutio vya watalii nalo liligusiwa na Wajumbe wengi. Kamati inaunga mkono hoja hii kwani itasaidia kuyaimarisha maeneo ya vivutio hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa muktadha huo, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha huduma za kijamii katika maeneo hayo kwa kuwekeza katika miundombinu ya maji safi na nishati endelevu. Hatua hii itahusisha kuimarisha usambazaji wa maji safi na

salama kwa kutumia teknolojia za kisasa za uchimbaji na kuhifadhi maji, pamoja na kuimarisha vyanzo vya nishati kama vile umeme na matumizi ya nishati mbadala kama vile jua na upepo. Uimarishaji wa huduma hizi kutawavutia watalii sambamba na kuimarisha ubora wa maisha ya wananchi, hivyo kuimarisha sekta ya utalii na uchumi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine ambalo limesisitizwa ni kuongeza wigo wa sekta ya utalii kwa kuanzisha na kuimarisha utalii wa michezo, utalii wa afya na utalii wa mikutano. Ili kuongeza wigo wa sekta ya utalii Zanzibar, Serikali inapaswa kuanzisha na kuimarisha utalii wa michezo, afya na mikutano. Serikali inaweza kujenga viwanja vya michezo vya kimataifa na kuandaa mashindano ya michezo ili kuvutia watalii wa michezo.

**Mheshimiwa Spika,** ni muhimu kuanzisha vituo vya huduma za afya za kibingwa na kuhamasisha matibabu maalum kama vile upasuaji na tiba za kisasa kwa watalii. Kwa utalii wa mikutano, Serikali inaweza kujenga kumbi za mikutano za kisasa na kuandaa mikutano na makongamano ya kimataifa. Hatua hizi zitapanua sekta ya utalii na kuongeza mapato.

**Mheshimiwa Spika,** Mataifa kama Dubai na Qatar yamefanikiwa katika utalii wa michezo, India, Afrika Kusini na Tunisia ni maarufu kwa utalii wa afya na Rwanda na Kenya kwa kiasi kikubwa zimefanikiwa katika utalii wa mikutano. Zanzibar tunaweza kujifunza kutoka kwa nchi hizi na kuchukua hatua zinazofaa.

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wengi wamezungumzia suala la kuimarisha utalii wa mirathi katika maeneo ya urithi wa asili kama vile makasri ya kale, mapango, mji mkongwe na makumbusho. Kamati inaishauri Serikali kuwekeza katika uhifadhi na uendelezaji wa maeneo hayo kwa kufanya ukarabati wa miundombinu na kutoa mafunzo kwa watunza makumbusho na kufanya kampeni za kimataifa za kutangaza urithi wa Zanzibar. Hivyo kuongeza idadi ya watalii na mapato ya sekta ya utalii.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaokuja katika nchi yetu Kamati inasisitiza juu ya usimamizi mzuri wa mapato yanayotokana na sekta ya utalii pamoja na kufungamanisha sekta hii na uchumi wetu. Kamati inaishauri Serikali kuiwekea mikakati madhubuti sekta ya utalii  kwani inatoa fursa kubwa ya kuimarisha mapato yetu na uchumi kwa ujumla.

## Ofisi ya Rais – Kazi , Uchumi na Uwekezaji

**Mheshimiwa Spika**, Miongoni mwa hoja ambayo imechukua muda mrefu katika majadiliano ya makadirio ya mapato na matumizi katika Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji ni kuhusiana na makusanyo ya kutoka Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuwawezesha vijana, wanawake pamoja na watu wenye ulemavu. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kusimamia taratibu za kuweza kutoa fedha hizo kwa makundi yaliyokusudiwa pamoja na kuwajengea uwezo wa namna ya kuzitumia na kuwaelimisha juu ya umuhimu wa kuzirudisha kwa wakati ili ziwanufaishe na wengine wanaohitaji.

**Mheshimiwa Spika**, Suala jengine ambalo Wajumbe walilichangia kwa msisitizo ni kuhusiana na Programu ya Usimamizi wa Sheria ya Kazi, Ukaguzi wa Kazi na Kazi za Staha kwa wote. Katika Programu hii Wajumbe walitaka kujua suluhisho la vijana ambao wanafanya kazi katika sekta binafsi na wanakosa stahiki zao ikiwemo kuvunjwa kwa mikataba bila utaratibu maalum, kutokupelekwa michango yao katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) licha ya kukatwa katika mishahara yao pamoja na mafao ya walioumia kazini. Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kuweka mikakati mahsusi ambayo itasaidia kutatua changamoto zinazowakabili vijana hao katika sehemu zao za kazi.

## Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

**Mheshimiwa Spika,** Katika Wizara ya Elimu na Mafunzo, Wajumbe walichangia kwa wingi kuhusu mtaala mpya wa elimu kwa ngazi ya elimu ya maandalizi na msingi. Licha ya kuwa majibu ya Serikali yametolewa kuhusiana na mikakati waliyoiweka kwa walimu ambao wamepatiwa mafunzo wa mtaala huo mpya, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha vitabu ambavyo vipo katika maandalizi ya uchapaji vinapatikana kwa haraka ili kuwawezesha wanafunzi kuvitumia kulingana na mabadiliko ya mtaala.

**Mheshimiwa Spika**, Eneo jengine ambalo Wajumbe walihoji ni kuhusu Posho za walimu ambazo kwa muda mrefu zimekuwa zikizungumzwa. Wizara ilieleza kwamba suala hili limeshafanyiwa marekebisho ambapo walimu watapata maslahi kwa mujibu wa ngazi zao. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuwapatia walimu stahiki zao kwa haraka ili suala hili likamilike utekelezaji wake.

## Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi

**Mheshimiwa Spika,** Kwa muda mrefu sasa suala la migogoro ya ardhi limekuwa likichukua muda katika majadiliano ya Bajeti za Wizara hii, Wajumbe huhitaji kujua hatua za utatuzi wa suala hili ili kuweza kupunguza kesi zinazotokana na migogoro ya ardhi. Kamati inaishauri Wizara kuandaa usimamizi mzuri ambao utasaidia kutatua changamoto hii kwa kiasi kikubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Ujenzi holela ni suala ambalo lilijadiliwa na Wajumbe wengi. kumekuwepo na ujenzi ambao haufuati taratibu za mipango miji. Licha ya kuwepo kwa suala la utambuzi wa ardhi ambalo litakwenda kusaidia jambo hili lakini pia Kamati inaitaka Wizara kuwashauri wananchi juu ya umuhimu wa upimaji wa ardhi ambao unafuata sheria na kufanya ujenzi kwa mujibu wa taratibu zinazotakiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Upatikanaji wa hati za kumiliki ardhi ni jambo lililojadiliwa kwa kina na wajumbe wengi. Kumekuwepo na malalamiko mengi kuhusu kutokupatikana kwa wakati kwa hati miliki ambapo huchelewesha ujenzi hususan katika baadhi ya miradi ambayo Kamati iliwahi kutembelea. Hivyo, Kamati inaisisitiza Wizara kuharakisha taratibu ambazo wameziweka ili kuhakikisha suala hili linafikia muafaka.

## Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo

**Mheshimiwa Spika,** Katika Wizara hii ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo michango ya Wajumbe wengi iligusia suala la Serikali kuwekeza fedha nyingi katika kilimo cha umwagiliaji kwa kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba. Kamati inaishauri Serikali kuweka mfumo thabiti wa ufuatiliaji na ukaguzi ili kuhakikisha kwamba miradi hii inatekelezwa kulingana na viwango vya ubora na ufanisi unaostahiki.

**Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi wa mara kwa mara unaweza kuhakikisha kuwa miundombinu inajengwa kwa kiwango bora. Serikali pia inapaswa kusaidia katika upatikanaji wa mbegu bora za mpunga kwa wakulima kwa bei nafuu au kwa kutoa ruzuku. Mbegu bora zitasaidia kuongeza uzalishaji na kufikia tija iliyokusudiwa. Hatua hizi zitasaidia kufikia tija iliyokusudiwa ya kuiwezesha Zanzibar kujitosheleza kwa chakula badala ya kuagiza bidhaa hizi nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Wajumbe wengi pia walichangia suala la kukosekana kwa nyenzo za kutendea kazi zikiwemo trekta ambazo zinatumika kulimia eneo kubwa kwa muda mfupi ili kuweza kupata uzalishaji mkubwa. Kamati inaungana na Wajumbe sambamba na kuishauri kuwapatia wakulima trekta na nyenzo nyengine za kilimo zikiwemo pembejeo ili kuzalisha mazao ambayo yatakwenda kuchangia katika kuinua hali za uchumi wa wananchi wanaotegemea kilimo na wa nchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaungana na Wajumbe waliozungumzia kuhusiana na uzalishaji wa zao la karafuu ambalo kwa sasa uzalishaji wake umekuwa ukishuka kadri siku zinavyosonga mbele. Miongoni mwa sababu za kuongezeka kwa Pato la Taifa ni uuzaji wa karafuu kwa nchi za nje. Kwa sasa zao hili linakumbana na changamoto nyingi ikiwemo mabadiliko ya tabianchi ambazo zinapelekea kushuka kwa kiwango cha uzalishaji. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizo na kuweka nguvu zaidi ya uzalishaji wa mazao mengine ambayo yatachangia katika kukuza Pato la Taifa.

**Wizara ya Afya**

**Mheshimiwa Spika**, Michango ya Wajumbe wengi katika Wizara ya Afya ilisisitiza suala la kuwepo kwa uhaba wa wakunga katika vituo vya afya na hospitali hali ambayo hupelekea kuzidiwa kwa wakunga waliopo katika utowaji wa huduma. Ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali kuongeza ajira za wakunga kwa kutoa nafasi zaidi za masomo na mafunzo ya uuguzi, kuimarisha mazingira ya kazi na maslahi ya wakunga ili kuvutia na kushikilia wataalamu zaidi katika sekta hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande mwengine Serikali ianzishe programu za muda mfupi za mafunzo kwa wakunga wapya na kutoa motisha kwa wakunga ili kuinua morali ya kazi ambayo itasaidia katika utoaji wa huduma kwa bidii kubwa. Hatua hizi zitasaidia kuboresha huduma kwa kina mama na kupunguza mzigo kwa wakunga waliopo.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine ambalo limesisitizwa ni upungufu wa madaktari na watendaji wengine wa afya katika hospitali zetu. Ili kukabiliana na tatizo hili, Kamati inaishauri Serikali kuwekeza katika elimu na mafunzo kwa kuongeza nafasi za masomo katika vyuo vya tiba na afya, pamoja na kutoa ufadhili na motisha kwa wanafunzi wanaochagua fani za afya. Pia, kuimarisha mazingira ya kazi na kuongeza

maslahi ya madaktari na watendaji wa afya kutasaidia kuvutia na kushikilia wataalamu waliyopo.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Serikali ihakikishe inaweka mkakati kwa wataalamu wetu wa afya wanapata fursa ya kusoma kwa vitendo utaalamu na ujuzi wa madaktari bingwa kutoka nje ya nchi wanaokuja Zanzibar kutoa huduma mbali mbali za kibingwa. Tusiishie kufaidika na huduma tu ya madaktari hao wa nje bali pia tufyonze ujuzi na maarifa yao kwani hilo ni la muhimu kwa sababu tutapata manufaa endelevu kwa kupitia madaktari wetu wa ndani.

**Mheshimiwa Spika,** Suala la kuimarisha Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF) pia limechangiwa na Wajumbe wengi. Serikali inapaswa kuchukua hatua madhubuti ili kuimarisha Mfuko huu. Kamati inaishauri Serikali, kuweka mifumo thabiti ya usimamizi na uwazi katika matumizi ya fedha za mfuko. Kutumia teknolojia za kisasa ili kuboresha usimamizi wa fedha na huduma, na kuhakikisha kwamba taarifa zinapatikana kwa wakati na kwa uwazi. Hatua hizi zitasaidia kuimarisha huduma za afya kwa wananchi na kuhakikisha ZHSF inaendelea kuwa na uwezo wa kukidhi mahitaji ya afya ya jamii.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine lililochangiwa na Wajumbe wengi katika Wizara hii ni kuchelewa kuanza kuwalipa Wafanyakazi wa Afya ya Jamii (CHW). Kwa vile katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha 2024/2025, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya shughuli hii, Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya utekekelezaji huo ili ufanyike kwa ufanisi. Hatua hii itasaidia kuimarisha huduma za afya katika jamii kwani Wafanya kazi wa Afya ya Jamii ni kiunganishi cha huduma za afya nje ya vituo vya afya sehemu zote wanazoishi wananchi.

## Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

**Mheshimiwa Spika,** Katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wajumbe wengi walisisitiza sana suala la vitendo vya udhalilishaji huku wakisikitishwa na namna kesi zake zinavyoendeshwa. Kamati inaishauri Wizara na Serikali kuendelea kushughulikia kesi zinazohusiana na udhalilishaji na kuhakikisha kuwa haki inatendeka kwa kuwajibisha wale wote wanaokutwa na makosa hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuwachukulia hatua watendaji wote wanaokwamisha uendeshaji wa kesi za udhalilishaji kwa maslahi yao binafsi. Sambamba na hayo, Serikali iimarishe mifumo ya msaada wa kisheria kwa waathirika wa udhalilishaji, ili kuhakikisha wanapata msaada wa haraka na wa kina wanapofungua kesi. Hii itajumuisha huduma za ushauri nasaha, ulinzi, na msaada wa kisheria bila malipo.

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wengi wameonesha masikitiko yao kutokana na kuwepo ongezeko la watoto wanaokinzana na sheria. Kamati inainasihi jamii kuendelea kuchukua juhudi zaidi katika kusimamia malezi ya watoto kuanzia katika ngazi za familia. Aidha, Kamati inaishauri Wizara katika kuwashughulikia watoto wanaokizana na sheria, itenge maeneo maalum kwa ajili ya watoto hao ili yaweze kuwasaidia katika kuwafundisha tabia njema na stadi nyengine za maisha.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine ambalo Wajumbe wengi walichangia ni kuhusiana na makaazi bora kwa wazee. Kamati inaunga mkono hoja ya Wajumbe za kuitaka Serikali kuimarisha makaazi ya wazee kwani ni muda wao wa kupumzika baada ya kuitumika nchi yetu kwa muda mrefu. Ili kufanikisha hili, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua madhubuti kuimarisha miundombinu na huduma katika makaazi ya wazee, ikiwemo upatikanaji wa huduma za afya, usalama, na mahitaji mengine muhimu, ili kuhakikisha wanaishi maisha bora na ya staha.

## Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi

**Mheshimiwa Spika**, Katika Wizara hii Wajumbe wengi walizungumzia sana suala la ukosefu wa boti kubwa na za kisasa ambazo zingewasaidia wavuvi wadogo wadogo ili kuweza kufika kina kirefu cha maji na kuvua samaki kwa uhakika. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kushughulikia changamoto hii kwa kuwekeza katika ununuzi na usambazaji wa boti hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kufanya hivyo, kutawawezesha wavuvi kuongeza ufanisi katika shughuli zao za uvuvi, hivyo kuimarisha kipato chao na kuinua uchumi wa jamii zao. Serikali ianze kutoa mafunzo ya matumizi salama na bora ya boti pamoja na kuweka mipango ya matengenezo na huduma kwa boti hizo ili kuhakikisha zinadumu kwa muda mrefu. Hatua hizi zitasaidia sana kuimarisha sekta ya uvuvi nchini na maisha ya wavuvi wadogo wadogo.

**Mheshimiwa Spika,** Suala jengine ambalo Wajumbe walilichangia sana na kwa msisitizo ni kuchukua muda mrefu mchakato wa uchimbaji wa mafuta na gesi. Kamati inaishauri Serikali kurahisisha taratibu za kisheria na kiutawala zinazohusiana na uchimbaji wa mafuta na gesi. Hii inaweza kutekelezwa kwa kuimarisha uwazi katika utoaji wa leseni na vibali, na kuanzisha mifumo ya kidijitali kwa ajili ya kusimamia taratibu hizi. Kamati pia inasisitiza umuhimu wa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mara kwa mara ya mchakato wa uchimbaji wa mafuta na gesi. Hii itasaidia kubaini changamoto zinazojitokeza na kuzitatua kwa wakati, pamoja na kuhakikisha kuwa shughuli hizi zinaendelea kwa ufanisi mkubwa.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mjadala wa kupitisha bajeti ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini Wajumbe wengi walichangia suala la kutopatikana kwa huduma ya maji kwa wananchi katika maeneo mengi. Licha ya Kamati kufahamu kwamba jitihada kubwa zimefanyika kwa kuimarisha miundombinu ya maji kama vile ujengaji wa matangi makubwa ya kuhifadhia maji pamoja na uchimbaji wa visima lakini kutokukamilika kwa miundombinu ya kuifikisha huduma ya maji katika maeneo ya wananchi inafanya kuwepo na malalamiko mengi. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha ukamilishaji wa miundombinu hii ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji kwa haraka na kwa uhakika.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine lilichochangiwa kwa msisitizo katika Wizara hii ni suala la kuchelewa kuungiwa umeme wananchi ambao tayari wameshalipia gharama za uingiwaji wa umeme. Aidha, Wajumbe wamechangia juu ya suala la umeme kuzimwa mara kwa mara na kupelekea usumbufu kwa wananchi. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuhakikisha wananchi waliyolipia huduma wanapatiwa huduma ya umeme bila kuchelewa. Pia, Serikali inapaswa kuweka mikakati madhubuti ya kuimarisha usambazaji wa umeme na kupunguza tatizo la umeme kuzimwa mara kwa mara. Hatua hizi ni muhimu kwani zitasaidia kuimarisha maisha ya wananchi, kukuza uchumi, na kuleta maendeleo endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine lililochangiwa na Wajumbe wengi ni suala la kuchelewa kuanza zoezi la ulipaji wa fidia kwa wananchi waliopoteza mali zao kutokana na kupisha miundombinu ya miradi wa maji na umeme. Kamati inaishauri

Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wanapatiwa fidia zao kwa wakati ili kufidia hasara walizopata. Ni muhimu kwa Serikali kuweka utaratibu wa wazi na wa haraka wa kulipa fidia hizo ili kuepusha malalamiko na kutokuwarudisha nyuma wananchi kiuchumi na kimaendeleo. Hatua hizi zitasaidia kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali na wananchi na kuhakikisha kuwa miradi ya maendeleo inatekelezwa kwa ufanisi na kwa usalama.

### Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda

**Mheshimiwa Spika**, Michango ya Wajumbe wengi katika Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ilisisitiza juu ya suala la kuwasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo kupata vifungashio bora vya kuweka bidhaa zao. Hatua hii itawawezesha wafanyabiashara hao kuimarisha ubora wa bidhaa zao na kuzifanya ziweze kushindana katika masoko ya kimataifa, hivyo kuwapa fursa ya kuuza bidhaa zao nje ya nchi. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha upatikanaji wa vifungashio bora kwa gharama nafuu kwa kushirikiana na sekta binafsi. Vilevile, Serikali inapaswa kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara wadogo kuhusu matumizi sahihi ya vifungashio hivyo na namna ya kusafirisha bidhaa zao nje ya nchi. Hatua hizi zitasaidia kuimarisha biashara za ndani na kuongeza Pato la Taifa kupitia mauzo ya nje.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Shirika la Biashara la Taifa la Zanzibar (ZSTC), Wajumbe wengi walichangia kuhusu mikakati ya kuongeza uzalishaji wa zao la karafuu. Uzalishaji wa zao la karafuu limekuwa likishuka kila mwaka. Kamati inaungana na Wajumbe kuishauri Serikali kufanya tafiti za kutosha ili kuweza vyanzo vinavyosababisha changamoto hiyo, na kwa kutumia matokeo ya tafiti hizo, Serikali inaweza kuandaa mipango ya kuimarisha uzalishaji wa karafuu na kuinua uchumi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**, Jambo jengine ambalo limesisitizwa ni suala la kujiendesha kwa hasara kwa Tawi la ZSTC lililopo Dar es Salaam. Kamati inapendekeza Serikali kuchukua hatua za haraka kuimarisha utendaji wa Tawi hili kwa kuhakikisha linauza bidhaa zinazotoka Zanzibar kama vile karafuu zilizotiwa katika vifungashio bora, mafuta ya karafuu, na bidhaa nyingine zinazozalishwa na Kiwanda cha Makonyo. Aidha, Tawi hili linapaswa pia kufanya biashara ya viungo vya chakula

vinavyozalishwa Zanzibar kama vile pilipili manga, mdalasini, uzile, na vyenginevyo. Hatua hizi zitasaidia kuongeza mapato ya Tawi hili, kukuza soko la bidhaa za Zanzibar, na kuhakikisha linaendeshwa kwa faida badala ya hasara. Ni Imani ya Kamati, iwapo Tawi litajishughulisha na uuzaji wa bidhaa hizi zinazozalishwa Zanzibar litaweza kupata faida kubwa na pia itafungua soko kwa bidhaa zetu.

**Mheshimiwa Spika**, Suala la mashirikiano baina ya Taasisi ya Viwango ya Zanzibar (ZBS) na Taasisi ya Viwango ya Tanzania (TBS) licha ya kuwepo kwa Hati ya Makubaliano (MOU) nalo lilichukua muda mrefu wa Wajumbe wengi kulichangia. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba mashirikiano kati ya taasisi hizi yanaimarishwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kuthibitishwa kwa ubora wa bidhaa zinazozalishwa Zanzibar na TBS kutasaidia bidhaa hizo kukidhi matakwa ya soko la nje ya nchi. Vilevile, mashirikiano haya yatasaidia kuongeza ufanisi wa kazi kwa ZBS kupitia hatua za ubadilishanaji wa uzoefu na utaalamu katika kazi. Serikali inapaswa kuchukua hatua za haraka kutatua changamoto zinazokwamisha ushirikiano huu na kuhakikisha utekelezaji wa MOU unafanyika kikamilifu.

## Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango Wajumbe wengi walichangia suala la kuimarisha mifumo itakayosaidia Taasisi za ukusanyaji wa kodi kukusanya mapato yatokanayo na sekta ya utalii kwa ufanisi. Licha ya kwamba idadi ya watalii wanaokuja Zanzibar imekuwa ikiongezeka lakini bado ukusanyaji wa mapato yake bado hajakusanywa kwa ufanisi. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka za kuweka mfumo mzuri wa kisheria na kiutawala ili kuhakikisha mapato ya utalii yanapatikana kikamilifu na kuchangia katika maendeleo ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapaswa kufanya uhakiki wa kina wa makampuni yote ya nje yanayoleta watalii Zanzibar ili kubaini mwenendo wa ulipaji kodi makampuni hayo na kuchukua hatua za kisheria kwa haraka pale inapostahiki. Aidha, Serikali iimarishe sheria za kodi ili kuzuia mianya ya ukwepaji wa kodi hususan katika hoteli za kitalii na kampuni zinazoleta watalii Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wengi pia walisisitiza suala la uhaba Dola za Marekani ambapo kumepelekea usumbufu kwa wafanyabiashara nchini wanapotaka kuagiza bidhaa nje ya nchi. Uhaba huu unaweza kuathiri vibaya shughuli za biashara na ukuaji wa uchumi kwa sababu biashara nyingi zinahitaji malipo kwa kutumia Dola za Marekani. Aidha, hali hii inaweza kusababisha kupanda kwa bei za bidhaa na kuathiri nguvu ya manunuzi ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhika na jitihada zinazochukuliwa na Serikali kukabiliana na changamoto hii, ikiwa ni pamoja na hatua za kudhibiti matumizi ya fedha za kigeni na kuhamasisha uzalishaji wa bidhaa za ndani ili kupunguza utegemezi wa uagizaji. Hata hivyo, ili kukabiliana na suala la uhaba wa Dola za Marekani kikamilifu, Kamati inaisisitiza Serikali kuendelea kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ili kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha upatikanaji wa kutosha wa fedha za kigeni, ikiwa ni pamoja na Dola za Marekani, ili kusaidia biashara na uagizaji wa bidhaa nje ya nchi hususan bidhaa za chakula. Hatua hii itasaidia kuhakikisha utulivu wa masoko ya fedha za kigeni na kurahisisha shughuli za ufanyaji wa biashara.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine ambalo limesisitizwa sana na Wajumbe wengi ni suala la upatikanaji mdogo wa fedha za matumizi mengineyo (OC) kwa Wizara na taasisi nyengine za Serikali. Changamoto hii inaweza kuathiri utekelezaji wa mipango na programu za Serikali kwa fedha hizi ndio hutumika katika uendeshaji wa taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha kwamba fedha za OC zinapatikana kwa wakati na kwa kiwango kinachostahili ili kuhakikisha utendaji mzuri wa shughuli za Serikali. Hii ni pamoja na kufanya tathmini ya mahitaji ya fedha za OC kwa kila Wizara na taasisi za Serikali, kuimarisha taratibu za upatikanaji na usambazaji wa fedha hizo, na kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za OC. Hatua hizi zitasaidia kuongeza ufanisi wa utendaji wa Serikali na kuhakikisha kuwa huduma muhimu zinapatikana kwa wananchi kwa wakati.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua fursa hii kwa mara nyengine kukushukuru kwa kunipa nafasi hii pamoja na kuwapongeza Mawaziri wote kwa uwasilishaji mzuri wa bajeti za wizara zao. Vilevile, napenda kutoa pongezi kwa Wajumbe wote kwa michango yao katika mijadala ya bajeti hizo. Michango yao kwa kiasi kikubwa imesaidia kuimarisha na hatimae kufanikisha kupitishwa kwa bajeti hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti ina matarajio makubwa kwamba Serikali itazingatia kwa umakini na kutekelezwa kwa ufanisi ushauri na maoni yote uliyotoa ili kusaidia kuimarisha mipango ya bajeti na kuwezesha maendeleo endelevu katika nyanja mbalimbali za kisekta.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunikisikiliza muda wote niliyotumia katika kuwasilisha Hotuba ya Kamati ya Bajeti kuhusu Majumuisho ya Mjadala wa Makadirio ya Bajeti kwa mwaka 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha.

Ahsante,

……………………………

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**